# FIDIA eNEWSLETTER

TOLEO LA NNE | OKTOBA - DESEMBA 2024 | www.wcf.go.tz



**TUCTA yaombwa kuhimiza waajiri kutoa taarifa WCF kuhusu wafanyakazi wanaoumia kazini.**
Uk. 6

**WCF yatoa elimu ya fidia kwa wamiliki na wafanyakazi wa viwanda**
Uk. 11

Scan kutembelea tovuti yetu

# MAJAJI MAHAKAMA YA RUFANI WATOA NASAHA KUZIDI KUIJENGA WCF

HABARI KAMILI Uk. 4

# UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU



**DKT. JOHN MDUMA**
Mkurugenzi Mkuu WCF

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuumaliza mwaka 2024 na kuuanza mwaka 2025 tukiwa wazima wa afya njema, na tuzidi kuwaombea wenzetu ambao wana changamoto za kiafya ili waweze kupona.

Wakati tunauanza mwaka huu mpya wa 2025, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wote wanaoshirikiana nasi katika kuhakikisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) unatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na uwazi. Napenda kuwahakikishia wadau wetu kuwa WCF utaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata magonjwa yanayotokana na kazi zao kwa mujibu wa sheria.

Tumefanya juhudi kubwa katika kuimarisha mifumo ya kielektroniki ili kurahisisha michakato ya fidia, kuboresha upatikanaji wa huduma kwa njia ya mtandao, na kufikisha elimu kwa waajiri na wafanyakazi kuhusu haki zao na wajibu wao chini ya mfuko huu.

Pamoja na mafanikio haya, tumeshuhudia changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo wa baadhi ya waajiri kuhusu umuhimu wa kujiunga na WCF. Hali hii imekuwa ni kikwazo kwa wafanyakazi wengi kushindwa kupata fidia wanapoumia au kupata magonjwa yanayotokana na kazi zao.

Hata hivyo, tunajivunia kuona kuwa WCF imeendelea kutoa elimu ya kutosha kwa waajiri, wafanyakazi, wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla, ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na jamii inayozingatia haki na maslahi ya wafanyakazi na kuhimiza waajiri kujiunga na WCF.

Aidha, napenda kuwashukuru watumishi wenzangu, waajiri na wadau wote kwa ushirikiano wenu thabiti. Kwa pamoja, tunaendelea kutimiza dhamira yetu ya kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote nchini wanapata haki zao wanapokutana na changamoto za ajali au magonjwa yanayotokana na kazi zao.

Mwisho nikukaribishe kusoma Toleo hili la Nne la Jarida letu la Fidia Mtandaoni, ambapo utapata fursa ya kufahamishwa kuhusu baadhi ya kazi na matukio mbalimbali ambayo WCF ilitekeleza na kushiriki katika kipindi cha kuanzia Mwezi Oktoba hadi Desemba 2024.

***Heri ya Mwaka Mpya.***

Scan kutembelea tovuti yetu

**Jarida hili limeandaliwa na**
**Kitengo cha Uhusiano kwa Umma WCF:**
**MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)**
**Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,**
**S. L. P 329, 41104 Dodoma,**
**TANZANIA.**

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

# 2025

HERI YA MWAKA MPYA

www.wcf.go.tz


FIDIA
eNewsletter
TOLEO LA TATU | JULAI-SEPTEMBA 2024

YALIYOMO
> WCF Yawagusa wakulima nchini
> Waziri Mkuu Majaliwa aipa kongole WCF kwa huduma bora
> Maafisa kazi watakiwa kutoa taarifa za wafanyakazi wanaoumia kazini

info@wcf.go.tz

## TIMU YA WAHARIRI


MWENYEKITI
**Dkt. John Mduma**

MHARIRI
**Laura Kunenge**

MHARIRI MSAIDIZI
**Mcharo Mrutu**

WACHANGIAJI
**Meseka Kadala**
**Sophia Mtakasimba**
**Lilian Shembilu**

# Majaji Mahakama ya Rufani watoa nasaha kuzidi kuijenga WCF



*Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Juma akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi baina ya Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania na WCF.*

*Na Mwandishi Wetu*

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Juma, amepongeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa kuendelea kutafuta maoni kuhusu sheria inayoisimamia Mfuko huo ili kuboresha utoaji wa fidia kwa wafanyakazi.

Jaji Mkuu alitoa wito huo wakati akifungua kikao kazi baina ya Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kilichofanyika Oktoba, 2024 mkoani Arusha.

Pamoja na pongezi hizo, Prof. Juma aliwahimiza waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania kuendelea kutoa ushauri wa kisheria utakaosaidia kufanyika kwa maboresho ya sheria Fidia kwa Wafanyakazi na hivyo kuongeza tija na ufanisi kwenye mnyororo wa utoaji haki kwa wafanyakazi wanaopata madhila yanayotokana na kazi zao.

"Tufahamu kwamba, ushirikiano kati ya Mahakama, Mfuko wa Fidia, na wadau wote katika mnyororo wa haki za wafanyakazi nchini ni sehemu ya Malengo ya Kikatiba ya Ustawi ya Jamii unaolenga kuhakikisha kuwa haki za wafanyakazi zinazingatiwa na kulindwa ipasavyo," ameongeza Jaji Mkuu.




*Picha ya pamoja kati ya Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahimu Juma, Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma na baadhi ya washiriki wa kikao kazi hicho.*

Kwa upande wake Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete akizungumza wakati wa kufunga kikaokazi hicho aliwahakikishia waheshimiwa Majaji hao kuwa mapendekezo wanayotoa ya uboreshaji wa sheria hizo yanapokelewa na kufanyiwa kazi.

"Eneo ambalo tunatamani zaidi kuendelea kupata mapendekezo yenu ni juu ya namna bora ya kuwahimiza waajiri ambao hawajajisajili WCF na kutowasilisha michango ya wafanyakazi wao kufanya hivyo bila kulazimishwa. Eneo hili ni muhimu sana kwani waajiri wasiotekeleza Sheria hiyo ya Fidia kwa Wafanyakazi wanakwamisha jitihada za Serikali katika kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanakuwa na uhakika wa kipato pale wanapopata ulemavu kutokana na ajali au magonjwa yanayotokana na kazi, au kwa wategemezi wao iwapo mfanyakazi atafariki kwa ajali au ugonjwa unaotokana na kazi,' alisema Waziri Kikwete.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma amesema kwamba ushirikiano baina ya Mfuko huo na Mahakama ya Tanzania umechangia katika maboresho kadhaa kuhusu Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ambapo pia michango ya waheshimiwa Majaji imehusika.

"WCF imeshiriki katika ufuatiliaji wa uboreshaji wa sheria mbalimbali kuhusu fidia ili kuongeza ustawi kwa wafanyakazi na familia zao na hatimaye kutunza nguvu kazi na kukuza uchumi wa Taifa kwa ujumla," alisema Dkt. Mduma.

Kikaokazi hicho pia kilihudhuriwa na Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu, Manaibu Wasajili wa Mahakama ya Rufani, Watendaji wa Mahakama, Makamishna wa Kazi kutoka bara na Zanzibar, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi pamoja na Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii.

# TUCTA yaombwa kuhimiza waajiri kutoa taarifa WCF kuhusu wafanyakazi wanaoumia kazini.




*Mkurugenzi wa Uendeshaji wa WCF, Bw. Anselim Peter akizungumza na washiriki wa Mkutano huo.*

*Na Mwandishi Wetu*

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umewaomba viongozi wa vyama vya wafanyakazi nchini kuwahimiza waajiri kuwasilisha taarifa mapema katika Mfuko huo pindi wafanyakazi wao wanapopata ajali au ugonjwa unaotokana na kazi zao ili kuharakisha upatikanaji wa fidia stahiki na kwa wakati ikiwemo fao la matibabu.

Ombi hilo limetolewa na Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Mfuko huo Bw. Anselim Peter alipokuwa akiwasilisha salamu za Mkurugenzi Mkuu wa WCF wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) uliofanyika Novemba 15, 2024 jijini




*Picha ya pamoja kati ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete na wadhamini wa Mkutano huo.*

Dodoma.
Bw. Peter alisema fidia zinazotolewa na Mfuko huo ni mtiririko wa mafao mbalimbali ikiwemo matibabu ambayo hayana ukomo, na kuongeza kuwa vyama vya wafanyakazi vina haki ya kutoa taarifa WCF kuhusu ajali au ugonjwa unaotokana na kazi endapo mwajairi atashindwa kufanya hivyo.

"Fidia ni mtiririko wa mafao, ambapo fao la kwanza ni la matibabu, sasa mtu akipata ajali au ugonjwa unatokana na kazi tunawaomba nyie muwe chachu ya kuwahimiza waajiri kutoa taarifa mapema WCF ili (mfanyakazi huyo) aweze kupata stahiki zake ikiwemo za matibabu. Matibabu haya yanaanzia katika hospitali zote ikiwemo kanda, taifa na hata nje ya nchi," alisema Bw. Peter.

Aidha, Bw. Peter amewataka pia viongozi hao wa vyama vya wafanyakazi kuwahimiza wafanyakazi wanaopata madhila wakiwa kazini kuwasilisha nyaraka kwa wakati ili Mfuko uweze kufanya tathmini mapema na wahusika walipwe fidia kwa wakati.

Mkurugenzi huyo ameongeza kuwa Mfuko umechukua hatua kadhaa kuhakikisha kuwa huduma zake zinapatikana kwa urahisi ikiwa ni pamoja na matumizi ya njia za mtandao ili kurahisisha utoaji wa huduma zake ikiwemo uwasilishaji wa taarifa na nyaraka muhimu.

"Tumeweka mifumo mbalimbali ya kielektroniki ili kurahisisha utoaji wa huduma zetu. Zaidi ya asilimia 90 ya huduma zetu zinapatikana kwa njia ya kielektroniki, ambapo mteja wetu anaweza kupata huduma zetu popote pale alipo," aliongeza Bw. Peter.




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (aliyevaa suti ya bluu) akizungumza jambo na Rais wa TUCTA Bw. Tumaini Nyamhokya (kushoto) mara baada ya kufungua Mkutano Mkuu wa Shirikisho hilo jijini Dodoma. Katikati yao ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa WCF, Bw. Anselim Peter (mwenye tai ya bluu). Wengine wanaoshuhudia ni baadhi ya viongozi wa TUCTA.*



# Madaktari waaswa kuwa sehemu ya utoaji wa fidia kwa wafanyakazi




*Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Paul Chacha akizungumza wakati akifungua mafunzo kwa madaktari kutoka mikoa ya Tabora, Kigoma, Singida na Dodoma kuhusu tathmini za ulemavu unaosababishwa na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi yaliyofanyika mkoani Tabora hivi karibuni.*

*Na Mwandishi Wetu*

**Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Paul Chacha ametoa wito kwa madaktari nchini kuwasaidia wafanyakazi wanaopata ajali au ugonjwa unaotokana na kazi zao kunufaika na huduma za fidia zinazotolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).**

**Mhe. Chacha alitoa rai hiyo wakati akifungua mafunzo kwa madaktari kutoka mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Tabora, Kigoma, Singida na Dodoma kuhusu tathmini za ulemavu unaosababishwa na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.**

**"Mkumbuke, utendaji wenu bora utasaidia wafanyakazi wanaopata madhila yanayotokana na kazi zao kufanyiwa tathmini za ulemavu kwa wakati, kulipwa fidia stahiki na kwa wakati, na hivyo kuweza kurejea kazini mapema kuendeleza uzalishaji na kukuza tija kwa Taifa" alisema Mhe. Chacha.**

**Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alitoa wito kwa madaktari wanaoshiriki mafunzo hayo kuwahudumia wateja wa Mfuko huo kwa uadilifu na kuwasaidia kukamilisha taratibu zinazohitajika na WCF ili waweze kupatiwa stahiki zao kwa wakati.**

**"Wito wangu kwa madaktari ni kuendelea kuwahudumia**




*Baadhi ya Madaktari wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zinawasilishwa katika mafunzo hayo*

wananchi kwa weledi na kama watagundua ugonjwa wa mfanyakazi umetokana na kazi yake basi wamsaidie kukamilisha taratibu zinazohitajika WCF ili aweze kugharamiwa matibabu na kufanyiwa tathmini ya ulemavu kama upo ili aweze kulipwa fidia stahiki na kwa wakati," alisema Dkt. Mduma.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tabora Dkt. Honoratha Rutatinisimbwa akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo aliwasisitiza madaktari kuwahudumia wagonjwa kwa weledi na kutoa taarifa za tathmini zinazotoa haki kwa pande zote, yaani wagonjwa, WCF na Serikali kwa ujumla.

"Ripoti zenu madaktari hasa za tahthmini ni muhimu sana kwani zitaisaidia WCF iweze kutoa haki kwa mhanga na pia kutosababisha hasara kwa Serikali," alisema Dkt. Honoratha.

Kwa upande wao baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo wamefurahishwa na utaratibu wa WCF kutoa mafunzo hayo kwa kuwa yatawaongezea ujuzi na uelewa juu ya huduma zinazotolewa na Mfuko huo na haswa fidia kwa wafanyakazi.

"Mafunzo haya yatatusaidia sisi madaktari kuwahudumia walengwa wa huduma zinazotolewa na WCF waliopo katika maeneo yetu ya kazi na hasa yale ya pembezoni," alisema Dkt. Kassim Kolola; huku Dkt. Margreth Kwai akisema "katika maeneo tunayoyahudumia wapo wafanyakazi wanaopata ajali au magonjwa yanayotokana na kazi zao, lakini wengi hawakuwa na uelewa namna ya kusaidika, hivyo mafunzo hayo yametujengea uelewa wa masuala mbalimbali kuhusiana na WCF pamoja na namna ya kufanya tathmini ya ulemavu".

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umejiwekea utaratibu wa kutoa mafunzo hayo kote nchini ili kuhakikisha wanufaika wa huduma zake wanahudumiwa ipasavyo, ambapo hadi sasa takribani madaktari 2,000 wemekwisha kupata mafunzo ya awali (general medical practitioners training) na madaktari wasiopungua 130 wamepata mafunzo hayo kwa vitendo (hands-on impairment assessment training).

# WCF yatoa elimu ya fidia kwa wamiliki na wafanyakazi wa viwanda




*Baadhi ya Wananchi waliojitokeza kwenye banda la WCF kupata huduma na elimu.*

*Na Mwandishi Wetu*

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetoa elimu kuhusu fidia kwa wafanyakazi kwa wamiliki na wafanyakazi wa viwanda walioshiriki na kutembelea Maonesho ya Nne ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mkoa wa Pwani ambayo yalizinduliwa rasmi na Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Suleiman Jafo.

Katika maonesho hayo, WCF ilitoa elimu kuhusu mafao yanayotolewa na Mfuko huo pamoja na huduma na taratibu za kufuatwa na waajiri na wafanyakazi ili kupata fidia stahiki na kwa wakati.

Mhe. Dkt. Jafo ambaye alipata fursa ya kutembelea banda la WCF akiambatana na Mwenyeji wake Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhe. Aboubakar Kunenge, ameipongeza WCF kwa kushiriki na kutoa elimu ya fidia kwa wananchi na hasa wafanyabiashara, waajiri na waajiriwa juu ya fidia kwa wafanyakazi.

"Ni vizuri WCF mmeshiriki katika maonesho haya ambayo yanahusisha wananchi wote na hasa wafanyabiashara na zaidi ya yote yamefanyika katika Mkoa wa Pwani wenye viwanda vingi ambavyo vinaajiri wafanyakazi wengi ambao WCF inawagusa moja kwa moja," amesema Mhe. Dkt. Jafo

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ni taasisi ya hifadhi ya Jamii inayohusika na kulipa fidia wafanyakazi pale wanapoumia au kuugua kutokana na kazi zao na pale bahati mbaya Mfanyakazi anapofariki kutokana na kazi, WCF inafidia wategemezi wake.

# WCF yaongeza juhudi za kulinda nguvu kazi Tanzania




*Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Peter Serukamba, akizungumza wakati wa akifungua mafunzo kuhusu tathmini ya ulemavu kwa madaktari kutoka mikoa ya Iringa, Njombe, Songwe, Rukwa, Mbeya, Katavi, na Ruvuma.*

*Na Mwandishi Wetu*

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Peter Serukamba, ameupongeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa juhudi zake katika kulinda nguvu kazi ya taifa kupitia ulipaji wa mafao ya fidia kwa wafanyakazi wanaopatwa na ajali au magonjwa yanayotokana na kazi.

Mkuu huyo wa Mkoa wa Iringa aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa madaktari kutoka mikoa ya Iringa, Njombe, Songwe, Rukwa, Mbeya, Katavi, na Ruvuma, yaliyofanyika mjini Iringa hivi karibuni. Mheshimiwa Serukamba amesisitiza umuhimu wa kuwajengea madaktari uelewa wa taratibu za kuwahudumia wanufaika mafao yanayotolewa na WCF.

Alisema, pamoja na manufaa mengine, mafunzo hayo yanasaidia kufanya tathmini ya athari za kibaolojia zinazotokana magonjwa na ajali za kikazi. "Nawashauri madaktari kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanapata huduma zinazostahili na fidia kwa wakati," alisisitiza Mkuu huyo wa Mkoa wa Iringa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisisitiza umuhimu wa waa-

jiri wote kujisajili na WCF kwa mujibu wa sheria na kufafanua kuwa lengo la Mfuko huo ni kulipa mafao kwa wafanyakazi wanaoumia kutokana na ajali au kuugua kutokana na kazi pamoja na kufidia wategemezi wa wafanyakazi pale watakapofariki.

Dkt. Mduma aliongeza kuwa katika kuhakikisha kuwa wanufaika wanapata huduma bora za afya, WCF imekuwa ikitoa mafunzo kwa madaktari kote nchini, ambapo hadi sasa madaktari 1,606 tayari wamepata mafunzo ya awali, na wengine 133 wamepata mafunzo ya vitendo.

Kwa upande wa madaktari waliohudhuria mafunzo hayo walisema semina hiyo inawawezesha kupata ujuzi wa kuhudumia wafanyakazi wanaopata changamoto za kiafya zinazotokana na kazi.




*Mhe. Peter Serukamba na Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma (wa pili kutoka kushoto) wakiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo.*



*Baadhi ya Madaktari wakifanya mafunzo kwa vitendo*

# Picha za Matukio mbalimbali













# Picha za Matukio mbalimbali















# KONA YA WANUFAIKA

*Ushuhuda wa Bw. Wilson Michael, mkazi wa Mwanza.*



Ushuhuda wa Bw. Wilson Michael, mkazi wa Mwanza. Simulizi ya Bw. Wilson Michael ni ushuhuda wa hali ngumu aliyoipitia baada ya kupata ajali akiwa kazini na msaada mkubwa wa mafao anaopatiwa na WCF.

***"nilipata ajali kubwa ya kuvunjika uti wa mgongo nilipokuwa ninatekeleza majukumu yangu ya kazi katika Daraja la Kigongo-Busisi"***

"Tarehe 22/7/2022 nilipata ajali kubwa ya kuvunjika uti wa mgongo nilipokuwa ninatekeleza majukumu yangu ya kazi katika Daraja la Kigongo-Busisi. Nilipata matibabu ya muda mrefu hospitalini, na nilijikuta nikihitaji msaada mkubwa kwa kuwa nilishindwa kurejea katika hali yangu ya kawaida."

Madaktari waliniambia: Wilson, maswahibu uliyoyapata ni makubwa, kwa hiyo huwezi kurejea katika hali yako ya kawaida, inabidi ukubali na uipokee hali yako mpya ili maisha yaweze kuendelea.

Kwa kweli, nilijawa na hofu na nilijiuliza, nitaishi vipi katika hali hii?

Hatahivyo, baada ya matibabu, nilitakiwa nipeleke vielelezo vya ajali yangu katika Ofisi za WCF. Nilipofanya hivyo, WCF ilianza kunihudumia pale alipoishia mwajiri wangu, na nilianza kupokea mafao ya kila mwezi mimi pamoja na msaidizi wangu. Pia, ninapata huduma ya msaada wa matibabu, jambo ambalo limekuwa faraja na msaada mkubwa sana kwangu na kwa familia yangu.

Nisingekuwa napata mafao haya ya WCF, ningejikuta nadhalilika na nimekuwa ombaomba barabarani. Sidhani kama kuna ndugu ambaye angeweza kunihudumia mimi na familia yangu."

Natoa wito kwa waajiri wote kujisajili na kuwasilisha michango yao WCF kwa wakati ili wafanyakazi wao wanapopata matatizo kama yangu waweze kunufaika. Hakuna mwajiri anayeweza kulipa mafao kama ambavyo WCF inalipa.

Hadi sasa, ni miaka miwili tangu nianze kupokea mafao haya, na najua kuwa nitaendelea kulipwa mafao haya kwa maisha yangu yote,".

Huu ni ushuhuda wa namna mafao ya WCF yanavyoweza kusababisha matumaini mapya kwa mfanyakazi aliyepatwa na madhila akiwa kazini.



# WCF kinara bonanza la ATE










*Na Mwandishi Wetu*

Timu za wanamichezo wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) zimeibuka vinara na kuzishinda timu za taasisi nyingine zilizoshiriki Bonanza la Waajiri lililoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) lililofanyika tarehe 19 Oktoba, 2024 katika Viwanja vya Michezo vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Timu za WCF zilizoibuka kidedea ni pamoja na timu ya Mpira wa kikapu, kuvuta kamba wanaume, kuvuta kamba wanawake, mchezo wa rede pamoja na mbio fupi.

# Happy Corner



Jarida hili limeandaliwa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma WCF:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S. L. P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA.

wcf_tz